- Kufanya jambo lolote ndani ya sheria kwa lengo la kuendeleza malengo ya kulinda, kumudu na kuleta matumizi adilifu na dumivu ya mazingira na rasilimali zake na kulinda na kukuza haki za binadamu.

UANACHAMA

Uanachama wa LEAT uko kwa wazi kwa asasi au mtu yeyote iwapo malengo ya asasi au mtu huyo yanafanana na malengo ya LEAT na ana nia ya dhati ya kulinda mazingira kwa vitendo. LEAT ina lengo la kuwajumuisha wataalamu na wajuzi wa kila aina ya fani kama wanasheria, wachumi, na wanasayansi ya jamii ambao wana nia na ari ya kweli ya kukuza umuduji dumivu wa mazingira na na maliasili nchini

Uanachama wa LEAT umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni uanachama wa kawaida na uanachama shirikishi.

MUUNDO:

LEAT inaongozwa na Timu ya Umuduji inayosimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji. Timu ya Umuduji inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa maelekezo kutoka Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Mkutano Mkuu wa Mwaka. Mkutano Mkuu wa Mwaka ndicho chombo kikuu cha maamuzi na utawala cha LEAT.

Kazi ya Timu ya Umuduji ni pamoja na:

- Kubuni na kutekeleza kazi, programu, mipango na miradi ya asasi;
- Kufuatilia maendeleo ya miradi na kupima matokeo ya utendaji kazi wa asasi;
- Kubuni njia za kuiingiza mapato asasi; na
- Kusimamia kazi mbalimbali za vikundi vya kijamii katika miradi husika.

MAHUSIANO NA ASASI NYINGINE:

LEAT inashirikiana na asasi mabalimbali ndani na nje ya nchi, ili mradi ziwe na malengo yanayofanana nayo. Kimataifa, LEAT inashirikiana na asasi iitwayo Environmental Law Alliance Worldwide (E-LAW) ambayo huwaunganisha wanamazingira wa masilahi ya watu duniani kwa njia ya baruameme, tovuti, kozi-fundishi na makongamano.

Aidha, LEAT inashirikana na taasisi iitwayo World Resources Institute (WRI), inayojihusisha na masuala ya mazingira ulimwenguni yenye makao yake makuu Jijini Washington, D.C USA; Shirika la Misaada ya Kimataifa la Marekani (USAID). LEAT ni mwananchama wa kinchi wa asasi ya utetezi wa mazingira duniani iitwayo Friends of the Earth (FOEI) na Friends of the Earth Africa.

Kitaifa, LEAT inashirikiana na Tanzania Media Fund (TMF), WCST, JET, TNRF, AGENDA for Sustainable Environment, ENVIROCARE, LHCR , HAKIARDHI, POLICY FORUM, Coalition for Human Right Defenders (HRD), Forum CC na nyingine nyingi zilizoko Dar es salaam na nje ya Dar es Salaam.

Kikanda, LEAT inashirikiana na asasi zisizo za kiserikali zenye malengo kama yake katika nchi za Afrika Mashariki mfano ILEG na RECONCILE za Kenya; ACODE na GreenWatch za Uganda; ZELA, ART na ZIM Trust za Zimbabwe, YONGENAWE ya Swaziland, Legal Resources Centre(LRC) ya Afrika Kusini.

ANUANI YETU:

Lawyers' Environmental Action Team
Jengo la Mazingira, Mtaa wa Mazingira
P.O. BOX 12605, Dar es Salaam
Tel: 255-22-2780859
Fax: 255-22-2780859
E-mail: info@leattz.org.
Website: http://www.leat.or.tz

Kitabupicha: Lawyers Environmental Action Team.

"AFRIKA YENYE MAZINGIRA NA MALIASILI DUMIVU ZINAZOMUDIWA VIZURI KWA VIZAZI VILIVYOPO NA VIJAVYO"

LAWYERS' ENVIRONMENTAL ACTION TEAM (LEAT)

(TIMU YA WANASHERIA WATETEZI WA MAZINGIRA KWA VITENDO)

LEAT NI NINI?

Neno LEAT ni kifupisho cha maneno ya Kiingereza 'Lawyers' Environmental Action Team' ambayo kwa Kiswahili ni "Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo.' LEAT ni asasi ya kiraia iliyoanzishwa mnamo mwaka 1994 na kusajiliwa rasmi mwaka 1995 kama asasi ya vyama vya kijamii. Mnamo Novemba 2001, LEAT ilibadili muundo wake na kuwa kampuni isiyokuwa na mtaji wa hisa chini ya Sheria ya Makampuni. Kwa usajili huo katika Sheria ya Makampuni LEAT ni asasi ya kiraia isiyotengeneza faida yenye kutetea na kukuza umuduji, ulinzi na matumizi dumivu ya mazingira na rasilimali zake.

DHAMIRA YA LEAT

LEAT ilianzishwa kutokana na kubaini mchango mkubwa na usio na kifani ambao wanasheria-mazingira kwa kushirikiana na wanamazingira wa kada na fani mbalimbali wanaweza kuchagiza na kuchukua hatua chanya za kukuza umuduji, utunzaji na ulinzi dumivu wa mazingira nchini. Ilipoanzishwa LEAT ndio ni taasisi ya kwanza yenye kupigania na kulinda masilahi ya watu ya kimazingira na maliasili nchini kwa kutumia mikakati ya kisheria, kisera na kiutetezi. LEAT Inafanya tafiti za kisera na kisheria, za umuduji na utunzaji na ulinzi wa mazingira kwa upande mmoja na kutetea na kushawishi katika mambo na masuala mbalimbali yenye masilahi ya watu na taifa na kufungua na kuendesha kesi zenye masilahi ya jamii na watu kwa niaba ya wananchi au mazingira.

DIRA YA LEAT

"Afrika yenye mazingira na maliasili dumivu zinazomudiwa vizuri kwa vizazi vilivyopo na vijavyo"

DHIMA YA LEAT

Kuchangia katika umuduji bora na matumizi dumivu ya mazingira na maliasili kwa kufungua na kuendesha kesi zenye masilahi ya jamii na watu, kufanya ushawishi na utetezi wa kimazingira na kimaliasili kwa upande mmoja na kufanya tafiti-mkakati na kuwajengea uwezo wananchi na kushirikiana nao kuleta mazingira dumivu pamoja na mfumo wa umuduji wake kwa upande mwingine.

MAADILI MUHIMU

LEAT inajihusisha kikamilifu katika kusimamia maadili yafuatayo:-

- Uaminifu;
- Uadilifu wa kweli;
- Utendaji kazi wa kitimu na kujitolea;
- Mapenzi ya kweli ya utetezi na ulinzi wa mazingira;
- Mwitikio wa wakati na Ufahamu;
- Kuheshimu na kulinda haki za binadamu; na
- Uwazi na uwajibikaji.

MWELEKEO

Kuleta ongezeko la uwezo na ushiriki wa wananchi wa Tanzania, Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika katika umuduji, utunzaji na ulinzi dumivu wa mazingira na maliasili, kwa kuzifahamu sera na sheria zinazohusu mazingira na maliasili, kukuza uwezo na mbinu zao kimikakati; na kushirikiana nao kupigania na kuleta umuduji dumivu wa mazingira na rasilimali zake.

MALENGO

Miongoni mwa malengo makuu ya LEAT ni pamoja na:

- Kuhakikisha kwamba demokrasia na haki inatumika katika maamuzi ya utunzaji na umuduji wa maliasili na mazingira nchini kwa faida ya Watanzania;
- Kuhakikisha wananchi wa Tanzania wanazielewa sera na sheria mbalimbali zinazohusiana na utunzaji, ulinzi, na umuduji mazingira na maliasili za nchi;
- Kufanya ukaguzi na uchunguzi wa kisheria kwa vitega uchumi vilivyopo na vinavyopendekezwa kuwekezwa nchini ili kuweka bayana faida na hasara za vitega uchumi hivyo kwa maisha ya wananchi na mazingira, na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kuwezesha wananchi wawe ndio wanufaikaji wakuu wa mazingira na rasilimali zake;
- Kushirikiana na wananchi katika matumizi dumivu na bora ya maliasili walizonazo na kujua haki zao juu ya maliasili hizo, ikiwa ni pamoja na haki ya kushiriki na kukuza uwezo wa jukumu lao katika utunzaji wa maliasili hizo;
- Kufanya tafiti za kisheria, kisera, kimazingira katika maswala mbalimbali ya mazingira na maliasili ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusiana na utawala, haki za binadamu, umiliki na upatikanaji wa chakula, mapambano dhidi ya umaskini na usawa katika jamii;
- Kushiriki na kuchangia katika mikakati mbalimbali ya kisheria na kitafiti katika ngazi za kimataifa na katika bara la Afrika na dunia kwa ujumla katika kulinda na kusimamia mazingira;
- Kuelimisha jamii na kuwafichua waharibifu wa mazingira na wakiukaji wa haki za binadamu na kuwashinikiza kisheria watendaji wa serikali kuwajibika kikamilifu katika kusimamia umuduji imara wa mazingira kwa upande mmoja na kufanya kampeni juu ya utunzaji na umuduji mzuri na dumivu wa mazingira kupitia semina, makongamano, vyombo vya habari, uenezi na utetezi, , pamoja na kuwanoa watoa maamuzi katika masuala ya mazingira juu ya umuhimu wa umuduji mzuri na dumivu wa mazingira kwa upande mwingine;
- Kushiriki, kuungana, kuunda au kujiunga na asasi za kiserikali au zisizo za kiserikali ambazo malengo yake yanafanana na malengo ya LEAT;
- Kukusanya, kusambaza na kuhifadhi taarifa zinazohusiana na sheria za mazingira za nchini nan chi mbalimbali na kuzisambaza kwa wananchi na wadau wengine; na